



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفَ  
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُكَلِّمُنَّهُمْ يَوْمَ دِينِهِمُ الَّذِي أَنْصَطْتُ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْفِهِمْ أَمْنًا  
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

### Taarifa kwa Vyombo vyahabari

#### **Ubepari ni Laana kwa Wanadamu wala sio Neema**

**(Imetafsiriwa)**

Huku Kenya ikigubikwa na mrundiko wa deni la jumla ya Sh.10 trillioni, Rais William Ruto awataka wakenya wawe wakilipa ushuru vilivyo. Kulingana na rais serikali inanuia kukusanya Sh.2 trillioni kwa mwaka ujao. Rais amewataka raia wawe na tabia ya kulipa ushuru ipasavyo ili kusaidia serikali kulipa deni lake na kuikomboa kutokana na zigo hili. Kwa sasa Serikali inatumia Sh.1 trillioni kulipia mikopo.

#### **Hizb ut-Tahrir Kenya ingependa kubaini yafuatayo:**

Deni la kitaifa lilokopwa kutoka mashirika ya kifedha ya kimataifa linazidi kuongezeka kila mwaka. Kenya inahitaji kwa sasa kukopa kitita cha Sh.900 bilioni kugharamikia mahitaji yake ya kifedha hatua ambayo ni suluhisho la muda ambalo kiuhalisia wake litaletia nchi masharti magumu yatakayodhalilisha zaidi na kujipata kwenye madeni zaidi hali itakayopelekea nchi kufilisika na hatimaye kujihatarisha zaidi. Ni bayana kwamba sera kandamizi zinazochukuliwa na serikali kutoka kwa shirika la IMF na Benki ya Dunia hubebesha raia mzigo mzito wa kiuchumi.

Chanzo muhimu cha kukusanya mapato ya serikali ndani ya Ubepari ni utozaji ushuru na ukopaji. Kulipisha ushuru matumizi na mapato ndio hufanya raia wa kawaida kulemewa katika harakati zao za kiuchumi siku baada ya siku kwani haya ndiyo mahitaji muhimu kwa maisha ya kila siku. Kama zilivyo tawala za kirasilimali, Kenya inafuata kile kiitwacho mfumo wa utozaji ushuru uliojikita zaidi kwenye utozaji wa ushuru kwenye mapato ya wafanyakazi na wafanyibashara. Ni wazi kwamba bajeti za kuendesha gharama za serikali ndani ya mfumo wa kibepari hutegemea pakubwa utozaji mkubwa wa ushuru huku nakisi kwenye bajeti ikisimamiwa na Mikopo na ruzuku.

Tunasema majiribio na juhudzi za serikali ya sasa yatazalisha madeni na hivyo kuzalisha majanga na kuwafanya raia wazidi kuumia kiuchumi.

Uislamu ndio suluhisho pekee la kumkomboa mwanadamu kwenye masaibu haya ya kiuchumi yaliyosheheni katika mfumo wa kirasilimali, hii ni kuwa Uislamu huhakikisha kwamba mali yote ya umma hutumika katika kuwashudumikia umma. Kipengele hiki Kimsingi kinaondoa kodi kama chanzo kikuu cha mapato hivyo kuacha matumizi na mapato yakisukumwa tu na nguvu za soko (mahitaji na usambazaji). Na kwa msingi huu, Dola ya Khilafah (Ukhalifa) kwa njia ya Utume ndiyo itakayo kuwa na uchumi wa kipekee utakaoweza kuwanasua wanadamu kwenye utumwa wa kiuchumi wa kikoloni wa dola za Magharibi.

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**